# KCPE 2000

## KISWAHILI

## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano:**
    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **21.** Fundi aliyachonga mawe
    A. huyu huyu
    B. haya haya
    C. hili hili
    D. hizi hizi.

    Jibu sahihi ni B.

    **Katika karatasi ya majibu:**

    **1** [A] [B] [C] [D]   **11** [A] [B] [C] [D]   **21** [A] ▬ [C] [D]   **31** [A] [B] [C] [D]   **41** [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Maswali 1 mpaka 15

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa maneno manne hapo. Chagua neno lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Bwana Masifa kila wakati alisikika akimsifu __1__ Pendo kuwa ni mtoto mwerevu, mtiifu na mwenye bidii. Masifa hakuwa na habari kuwa Pendo alikuwa hasomi ila __2__ muziki wa redio. Mwisho wa muhula alidai kwamba alikuwa wa kwanza __3__ hakuonyesha ripoti. Baba alisema, "Hongera Pendo, __4__ enzi zangu za zamani. Sikukubali mwanafunzi mwingine yeyote kunipita. Nilishikilia nambari ya kwanza kama wewe nyakati __5__. Pendo kwa kiburi __6__ kimoyomoyo, "Mnhu, si uongo tu, hiyo ni lugha ya kila mzazi."

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. mwanawe | B. mwanako | C. mwenetu | D. mwanangu |
| **2.** | A. kujisikia | B. kujishikilizia | C. kujisikilizia | D. kusikilizia |
| **3.** | A. kwa vile | B. ingawa | C. ikawa | D. kwa sababu |
| **4.** | A. unakumbukia | B. unanikumbushia | C. unanikumbukia | D. unanikumbusha |
| **5.** | A. yote | B. zozote | C. zote | D. yoyote |
| **6.** | A. akajisemea | B. akasemea | C. akajisema | D. akasemesha |

Siku moja, mambo __7__ walimu kooni. Wakapeleka ujumbe wa haraka wazazi __8__. Mara walipopiga hodi __9__ ya mwalimu __10__ butwaa kusikia kinyume cha mambo. Waliambiwa kuwa kwa muda mrefu Pendo amekuwa __11__ na amekuwa akiburuza mkia darasani. Hawakuamini lakini mtoto __12__ mbele yao __13__. Pendo hakufaulu maishani na wazazi walijuta kwa __14__ udongo __15__ maji.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| **7.** | A. yaliwafikisha | B. yaliwafika | C. yaliwafikia | D. yalimfika |
| **8.** | A. wajie | B. wamjie | C. watujie | D. waje |
| **9.** | A. kwa ofisi | B. karibu na ofisi | C. kwenye ofisi | D. karibu ofisini |
| **10.** | A. walikamatwa na | B. walisikia | C. walihisi | D. walipigwa na |
| **11.** | A. jeuri | B. kijeuri | C. ujeuri | D. vijeuri |
| **12.** | A. aliitwa | B. alipoitwa | C. akaitwa | D. aliyeitwa |
| **13.** | A. aliungana | B. aliunga | C. aliungama | D. aliandama |
| **14.** | A. kutomuwahi | B. kuuwahi | C. kumuwahi | D. kutouwahi |
| **15.** | A. wenye | B. ungali | C. una | D. uko |

**Kutoka swali la 16 mpaka 30 chagua jibu lililo sahihi.**

16. Chagua neno lifaalo:

_________ aliposikia kukibishwa hodi, alisimama na kuelekea mlangoni.
   A. Pindi
   B. Kwani
   C. Baada
   D. Kuwa

17. Jaza pengo kwa neno mwafaka.
Babu ___________ njia hadi nyumbani kwake.
   A. alisindikizwa
   B. aliongozana
   C. alishikwa
   D. aliongoza

18. Chagua wingi wa
'Kitabu changu kizuri kimeraruliwa'.
   A. Vitabu zangu nzuri vimeraruliwa.
   B. Vitabu vyangu vizuri vimeraruliwa.
   C. Vitabu vyetu vizuri vimeraruliwa.
   D. Vitabu vyetu zuri zimeraruliwa.

19. ___________ kwa wale wezi hakungeweza kuwafanya wasamehewe.
   A. Kutetea
   B. Kujitetea
   C. Kuitetea
   D. Kuzitetea

20. Viazi vyake ___________ gari.
   A. vilichukuliwa kwa
   B. vilichukuliwa na
   C. vilibebwa na
   D. vilibeba kwa

21. Ni maneno yapi ambayo yote ni vielezi?
   A. Rasmi, Kitunguu, Kiziwi, Safi.
   B. Mzuri, Mweupe, Yeyote, Pale.
   C. Upesi, Kitajiri, Sana, Kivivu.
   D. Muungwana, Mwerevu, Kimaskini, Gunia.

22. Ukubwa wa sentensi 'Kitoto kilivaa kijikanzu cheupe' ni
   A. Mtoto alivaa kanzu jeupe.
   B. Mtoto alivaa kanzu nyeupe.
   C. Toto lilivaa jikanzu nyeupe.
   D. Toto lilivaa jikanzu jeupe.

23. Chagua sentensi iliyo sahihi kisarufi.
   A. Michuzi yote mingine zilikuwa na chumvi isipokuwa hii.
   B. Michuzi yote mingine ilikuwa na chumvi isipokuwa huu.
   C. Michuzi yote mingine ilikuwa na chumvi isipokuwa hizi.
   D. Michuzi yote mingine mlikuwa na chumvi isipokuwa hizi.

24. Ni sentensi ipi inayoonyesha hali ya kufanyiza?
   A. Mbwa anaogopewa.
   B. Mbwa anaogopea.
   C. Mbwa anaogopeka.
   D. Mbwa anaogofya.

25. Chagua mpangilio unaofaa zaidi.
   A. Wageni walipowasili niliwalaki, nikawapokea mizigo na nikawakaribisha wakaketi.
   B. Niliwalaki nikawapokea mizigo, wageni walipowasili na nikawakaribisha wakaketi.
   C. Wageni walipowasili nikawakaribisha wakaketi, niliwalaki na nikawapokea mizigo.
   D. Niliwalaki na nikawakaribisha wakaketi, nikawapokea mizigo wageni walipowasili.

26. Mfano wa kiashiria hapa ni:
   A. Ndivyo.
   B. Ambaye.
   C. Hicho.
   D. Bali.

27. Neno <u>wayu</u> liko katika ngeli ya:
   A. M-Wa.
   B. U-N.
   C. M-Mi.
   D. N.

28. Rangi ya hudhurungi ni sawa na:
   A. rangi ya zambarau
   B. rangi ya kijivu
   C. rangi ya kahawia
   D. rangi ya manjano.

29. Malizia methali:
Siri ya mtungi ___________
   A. ajuaye kopo
   B. ajuaye chungu
   C. ajuaye debe
   D. ajuaye kata.

30. Chagua umoja wa sentensi:
Hawa nao ndio waliopita kama sisi.
   A. Huyu naye ndiye aliyepita kama mimi.
   B. Huyu naye ndiye aliyempita kama sisi.
   C. Huyu naye ndio waliyempita kama sisi.
   D. Huyu nao ndio waliyepita kama mimi.

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.**

Ama kwa hakika katika mwongo huu wa kufunga karne ya ishirini tumeshuhudia dunia yetu ikicharazwa kwa mikasa mithili ya mtoto aliyepotoka aadhibiwavyo na mzazi. Kadri upotoTu wa mtoto uendeleavyo kuongezeka ndivyo adhabu nayo inavyoongezeka mpaka mabadiliko mema yapatikane.

Si jambo la mjadala tena kusema kuwa kwa jumla walimwengu wa sasa ni wapotovu kuliko wale wa miaka hamsini iliyopita. Licha ya hivyo misikiti na makanisa hujaa waumini tele. Hawa husomewa maandishi matakatifu na kusisitiziwa umuhimu wa maadili kila mara. Inaonekana ni kweli sikio la kufa halisikii dawa.

Je, kuna uhusiano kati ya kudidimia kwa uadilifu na mikasa iliyokumba dunia yetu katika mwongo huu? Watu wengi wanaamini upo uhusiano.

Nchi ya Marekani katika jimbo la California barabara moja kuu ilipasuliwa na mtetemeko mkubwa wa ardhi. Watu waliokuwa katika safari zao wakaangamia. Baadaye mji wa Kobe kule Ujapani uliharibiwa sana na mtetemeko mwingine. Mwaka jana sehemu ya kaskazini mwa Uturuki ilikumbwa na balaa ii hii na maelfu ya watu wakafariki; hatutaji maelfu walioachwa bila makao. Baadaye nchi jirani ya Ugiriki ilipata maafa kama hayo.

Ni nani asiyekumbuka gharika iliyoenea Marekani ya kati mwaka huo huo? Mito ilifurika kutokana na mvua kubwa, maji yakaleta maafa makubwa nchini Guatemala, Nicaragua na kwingineko.

Nchi za Ulaya nazo zilipatwa na janga tofauti. Katika majira ya kiangazi baadhi ya nchi zilizidiwa na joto. Katika Uhispania na Ufaransa iliwabidi watu wengi wahame makazi yao wakimbilie sehemu zenye milima angalau wapate nafuu ya baridi.

Bara la Afrika nalo halikubahatika. Mvua kubwa ambayo haijawahi kunyesha kwa miongo ya miaka imewaua mamia ya watu Afrika Kusini na Msumbiji katika mwaka wa elfu mbili.

**31.** Neno jingine lenye maana ya <u>mwongo</u> ni
A. mia.
B. kumi.
C. elfu.
D. hamsini.

**32.** Mabadiliko mema ya mtoto mpotovu
A. huzidisha adhabu
B. huendeleza upotovu
C. huendeleza adhabu
D. hupunguza adhabu.

**33.** 'Si jambo la mjadala tena' ina maana kuwa:
A. Si swala la kubishaniwa.
B. Si swala lenye maana.
C. Si swala la kutangaziwa.
D. Si swala lenye masharti.

**34.** Uovu umeendelea duniani hata baada ya:
A. makanisa na misikiti kuongezeka
B. wakristo na Waislamu kuelewana
C. waumini wa dini kuongezeka
D. waumini wa uongo kupungua.

**35.** Maana ya methali 'sikio la kufa halisikii dawa' ni:
A. Asiyesikia hasikii.
B. Asiyetii ni vigumu kumkanya.
C. Sikio la kufa halitibiwi.
D. Asiyesikia haambiwi.

**36.** Mwandishi anaamini kuwa:
A. hakuna uhusiano kati ya uovu na maafa
B. hakuna uhusiano kati ya dini na maafa
C. kuna uhusiano kati ya uovu na maafa
D. kuna uhusiano kati ya dini na maafa.

**37.** Mitetemeko ya ardhi iliharibu
A. sehemu za Uturuki, California na Ugiriki.
B. sehemu za Ujapani, Guatemala na Nicaragua.
C. sehemu za California, Ujapani na Guatemala.
D. sehemu za California, Ugiriki na Guatemala.

**38.** Mafuriko yaliyoenea Marekani ya kati yalitokana na
A. mawimbi ya baharini
B. mvua ya rasharasha
C. mawimbi ya upepo
D. mvua ya gharika.

**39.** Iliwabidi Wazungu wakimbie makwao ili wajinusuru kutokana na
A. baridi
B. mvua
C. joto
D. mitetemeko.

**40.** Nchi mbili zilizoathiriwa na mvua ni
A. Uturuki na Ugiriki
B. Msumbiji na Afrika Kusini
C. Ujapani na Msumbiji
D. Guatemala na Ujapani.

**Soma habari ifuatayo kisha ajibu maswali 41 mpaka 50.**

Hapo zamani za kale paliishi mtumwa mmoja ambaye alidhulumiwa sana na tajiri wake. Licha ya kufanyishwa kazi za sulubu kutwa kucha, alicharazwa kwa mijeledi. Mtumwa huyu jina Hashimu hakuweza kustahimili tena mateso haya. Alipiga moyo konde, akaamua kutorokea kokote kule, na liwe liwalo. '<u>Nitaacha kasri hili la shakawa</u> na kutafuta usalama kokote. Hapo nitakuwa huru na jitu hili katili halitaweza kuniona tena.'

Hashimu alijua kwamba alihitaji ujasiri na uangalifu mwingi. Bila ya hayo mpango wake <u>ungetumbukia nyongo</u>. Basi siku moja alingojea mpaka giza tororo lilipoukumbatia usiku, kisha akatoroka bila kuonekana na yeyote. Alipofika mbali na kasri hilo alikimbia kwa mbio za farasi mpaka akafika katika msitu uliojaa miti kochokocho. Alipiga milundi kwa muda wa siku nyingi asipate hata mhisani mmoja, lakini haya yote hayakumfanya <u>kughairi</u>. Nguo zake zilichanwa na miiba na matawi ya miti. Njaa nayo ilimbana kwelikweli.

Ghafla, aliona pango kubwa karibu naye. Akashusha pumzi akasema, 'Hatimaye nimepata mahali pazuri pa pumziko. Huyo mjalaana hatanipata.' Hashimu aliingia pangoni, akawa yu hoi kwa uchovu. Mara akaanza kusinzia na kulala <u>usingizi wa pono</u>. Muda si muda aliamshwa na mngurumo mkali uliosikika kama radi. Humo mdomoni mwa pango mlisimama mfalme wa hayawani – simba. Akaanza kumkabili Hashimu. Kijasho chembamba kilianza kumtiririka huku akitamani ardhi ipasuke aingie. Hashimu alitetemeka kwa hofu alipoona jinyama hilo likimkaribia huku likiinua guu lake la kushoto. Lilinguruma kwa maumivu, kuonyesha kuwa lilihitaji kuauniwa. Hashimu alimeza mrututu na kuamua kulisaidia kwa kuung'oa mwiba uliokuwa umelichoma guuni. Simba alivaa tabasamu na kutikisa mkia wake kumshukuru Hashimu.

Tangu siku hiyo Hashimu na simba wakawa marafiki wa kufa kuzikana. Waliishi pamoja kwa muda mrefu huku simba akimfadhili kwa mawindo. Usiku Hashimu na sahibu wake walilala pamoja pangoni, simba akililinda pango hilo.

**41.** Kwa nini Hashimu aliamua kutoroka?
A. Alipewa chakula na kudhulumiwa na tajiri wake.
B. Alitamani kuonana na rafikiye.
C. Alichoshwa na maisha ya upweke.
D. Alidhulumiwa kwa kazi nyingi na kuchapwa.

**42.** Maana ya '<u>Nitaacha kasri hili la shakawa</u>' ni
A. Nitaacha jumba hili la fahari lililojaa shida.
B. Nitaacha jumba hili kubwa la fahari lililojaa raha.
C. Nitaacha maisha haya ya shida.
D. Nitaacha jumba hili la mfalme.

**43.** Hashimu alitoroka wakati gani?
A. Usiku ulipoanza
B. Alfajiri na mapema.
C. Usiku wa manane.
D. Usiku wa giza jingi.

**44.** Maana ya '<u>ungetumbukia nyongo</u>' ni
A. ungeangukia nyongo
B. ungetengenezeka
C. ungeharibika
D. ungekuja kuchelewa.

**45.** Maana ya '<u>kughairi</u>' ni
A. kubadili nia
B. kufa moyo
C. kuogopa sana
D. kupunguza mwendo.

**46.** Mfalme wa hayawani alionyesha vipi kuwa alihitaji usaidizi?
A. Kwa kunguruma kwa ukali.
B. Kwa kumkabili Hashimu.
C. Kwa kuinua guu lake la kushoto na kunguruma.
D. Kwa kuinua mguu wake wa kulia na kunguruma.

**47.** Maana ya '<u>usingizi wa pono</u>' ni
A. usingizi mwepesi
B. usingizi mzito
C. usingizi wa shida
D. usingizi wa mang'amung'amu.

**48.** Hashimu alionyesha wema upi kwa mnyama huyu?
A. Alimchungia pango.
B. Alimsaidia kuwinda.
C. Kwa kumpapasapapasa.
D. Alimng'oa mwiba.

**49.** Methali 'wema hauozi' imedhihirika vipi katika habari hii?
A. Simba alimfadhili Hashimu baadaye.
B. Simba alimsaidia Hashimu baadaye.
C. Simba alimpatia Hashimu makao mazuri.
D. Simba alimwonea Hashimu imani.

**50.** Chagua kichwa kinachofaa zaidi kwa kifungu hiki.
A. Hashimu na simba pangoni.
B. Mateso ya Hashimu.
C. Kasri la shakawa.
D. Ukarimu wa simba.